

Maswali

1. Mfalme wa Moabu aliitwa nani?
2. Waisraeli walimtumikia kwa miaka mingapi?
3. Muamuzi yupi alitumwa na Mungu awaokoe Waisraeli?
4. Mfalme wa Moabu aliuwawa na nini?
5. Mbona Mungu alikubali Wamoabu wawatawale Waisraeli?
6. Mbona watumishi wa mfalme hawakuzuia asiuwawe?
7. Ehudi alitorokea wapi?
8. Ehudi aliwaita Waisraeli namna gani?
9. Baada ya hayo Waisraeli walikuwa na amani kwa mda gani?
10. Tunajifunza nini kwa hadithi hii?

Majibu

1. Egloni.
2. Miaka 18.
3. Ehudi
4. Upanga wa makali kuwili.
5. Waisraeli waliasi Mungu kwa kuabudu miungu za uongo.
6. Egloni aliwatoa watumishi wake nje.
7. Vilima vya Efraimu katika Israeli.
8. Ehudi alipiga tarumbeta.
9. Miaka 80.
10. Kila wakati tukitubu dhambi zetu Mungu hutusamehe.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



9 Hadithi ya Egloni

Marejeo

Waamuzi 3:12—30

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ni mvumilivu na tukitubu hutusamehe wakati wowote

Maneno maalum


1. Israeli + Waamuzi + Egloni + Moabu
2. Miaka 18 ya shida + maombi + Ehudi + mtu wa kushoto
3. Zawadi + makali kuwili + ujumbe wa siri
4. Upanga + mtu mnono + Ehudi + heba + Egloni + kufa
5. Kilima cha Efraimu + tarumbeta + vita + amani + miaka 80
6. Mungu + msamaha + saidia

9.1 Hadithi hii ilifanyika wakati Israeli ilitawaliwa na Waamuzi. Waisraeli, watu waliochaguliwa na Mungu walikuwa wakiishi kwa nchi waliyopewa na Mungu. Walizungukwa na mataifa mengine waitwao Wahiti, Waperizi, Wahivi na Wayebusi. Waisreili walikuwa wameanza kuabudu miungu ya watu hawa. Wameoa wanawake wao na hali Mungu aliwasurutisha wasiwaoe. Hii ilimkasirisha Mungu na akaamua asaidie Egloni mfalme wa Moabu na mataifa mengine kuwashambulia Israeli.


9.2 Walipigana Waisraeli wakashindwa na Egloni na kumtumikia kwa miaka 18. Baada ya hizo miaka zilizokuwa za shida Waisraeli walimlilia Mungu awaokoe. Mara tena Mungu alijibu maombi yao na akawaleta muamuzi awaokoe. Muamuzi aliyechakuliwa na Mungu alitwa Ehudi mwana wa Gera Mbenyamini. Mtu aliyetumia kushoto. Lakini angemfikia Egloni namna gani ili amuue? Kwa hivyo akawa na mpango.

9.3 Egloni aliwalazimisha Waisraeli wamlipe pesa kila mwaka kama ushuru. Kabla Ehudi hajampelekea ushuru, alitengeneza upanga mfupi wa makali kuwili na kuuficha ndani ya koti lake.

Ehudi alipoenda kumuona mfalme Egloni, alikuwa amekaa kwa chumba cha baridi cha kifalme. Baada ya Ehudi kumpa mfalme Egloni pesa aliwambia watu wengine watoke. Alisema kwamba alikuwa na ujumbe wa siri kwa mfalme. Mfalme aliwambia wafanya kazi watoke na wabaki na Ehudi pekee yake.



9.4 Mfalme alipotaka kuinuka ili azungumze na Ehudi, Ehudi alitoa upanga kutoka kwa koti na kumtunga tumboni. Mfalme Egloni alikuwa mnono na bunde tu mafuta yalifunikia upanga ndani ya tumbo usiweze kuonekana. Ehudi alitoka haraka na kufunga mlango nyuma yake. Alitoka kwa hiyo nyumba ya kifalme na kurudi Israeli. Wafanya kazi wa mfalme Egloni walingoja hapo nje mpaka wakaanza kuwa na wasiwasi. Hatimae walifungua mlango na kuona mfalme Egloni sakafuni amekufa.



9.5 Ehudi alitorokea Israeli na akaenda kwa vilima vya Efraimu. Akiwa kule alipiga tarumbeta ya kuita Waisraeli. Aliwambia watu kwamba Mungu amewaokoa kutoka kwa Wamoabu. Akawaongoza kupigana na Wamoabu. Mungu aliwasaidia wakaua jeshi la Moabu watu 10,000. Kutoka hapo, Wamoabu walikuwa watumishi wa Israeli kwa miaka 80.

9.6 Hadithi hii inatufundisha kwamba tukimrudia Mungu na tuombe msamaha vile Wasraeli wilifanya, atatusaidia katika maisha yetu sawa sawa alivyowasaidia Waisraeli kushindana na Moabu.